MAELEZO YA JUMLA KUHUSU PROGRAMU YA TANZANIA YA MPANGO WA CHANGAMOTO YA MILENIA (MILLENNIUM CHALLENGE ACCOUNT TANZANIA)

1.0 UTANGULIZI

Mfuko wa Changamoto ya Milenia (Millennium Challenge Account) ni mpango maalum ulianzishwa na Serikali ya Marekani mwaka 2004 kama sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Rais Bush wa Marekani katika Mkutano wa Kimataifa wa "Monterrey" wa mwaka 2002. Mfuko huu unatoa msaada wa fedha kwa ajili ya kuchochea maendeleo na kuboresha maisha ya wananchi katika nchi maskini zinazoonesha jitihada kubwa ya kujenga uchumi imara na endelevu, kuongeza kipato cha wananchi wake na hivyo kuwa katika nafasi nzuri ya kuboresha maisha ya watu wake. Kazi ya kuandaa miradi inayofadhiliwa na mfuko huu ni jukumu la nchi inayohusika. Hata hivyo kuna utaratibu maalum wa kufuata wakati wa maandalizi ya mapendekezo ya nchi.

Ili kusimamia vizuri Mfuko huu Serikali ya Marekani ilianzisha shirika lijulikanalo kama Millennium Challenge Corporation (MCC) mwaka 2004. Shirika hili linaongozwa na Mtedaji Mkuu aliyeteuliwa na Rais wa Marekani na linasimamiwa na Bodi ambayo mwenyekiti wake kwa sasa ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani. Shirika hili ndilo linalotoa miongozo mbalimbali na kusimamia maandalizi na utekelezaji wa programu za nchi zilizoingia katika mpango huu. Mtendaji Mkuu wa Shirika aliitembelea Tanzania na Kukutana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vilevile Rais wa Zanzibar Mwezi Januari mwaka huu 2007.

Tanzania ilikubaliwa kushiriki kwenye mpango huu mwezi Novemba mwaka 2005 baada ya kufuzu vigezo muhimu vinavyotumika kupima nchi zinazowania kuingia katika mpango huu. Kufuatia mashauriano yaliyofuatia uamuzi huu, mapema mwaka 2006, Makamu wa Rais wa Shirika la Millenniun Challenge Corporation (MCC) aliitembelea Tanzania kwa lengo la kueleza shughuli za Shirika hilo na mchakato mzima wa mpango huu. Vile vile, maelezo ya kina yalitolewa kuhusu masharti yanayotakiwa yazingatiwe.

Programu ya Tanzania kuhusu Mpango wa MCA inaandaliwa kufuatana na miongozo ya MCC. Programu hii ni mojawapo ya programu za utekelezaji wa Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania yaani MKUKUTA kwa Tanzania Bara na MKUZA kwa upande wa Zanzibar.

2.0 MCHAKATO WA MCA

Utaratibu mzima ni mrefu na unahitaji ushirikishwaji wa wadau wengi zikiwemo taasisi mbalimbali za serikali, mashirika ya hiari na sekta binafsi. Kuna hatua 5 muhimu za mchakato huu:-

2.1 Hatua ya kwanza ni kufuzu na kuingia katika mpango huu.

Vigezo vinavyotumika kupima nchi kwa lengo la kuziingiza katika mpango huu viko katika mafungu 3 yaani:

i) Utawala mzuri na wa haki
ii) Uwekezaji katika rasilimali watu
iii) Uhuru katika shughuli za kiuchumi

Ili nchi iweze kuingia katika mpango huu inapaswa kushinda zaidi ya nusu ya viashiria vinavyotumika kupima tatizo la rushwa, na angalau nusu ya viashiria 16 vingine vinavyotumika katika maeneo hayo matatu yaani:

- Utawala mzuri na wa haki (nchi ishinde viashiria 3 kati ya 6)
- Uwekezaji katika rasilimali watu (viashiria 2 kati ya 4)
- Uhuru katika shughuli za kiuchumi (viashiria 3 kati ya 6)

2.2 Hatua ya pili ni maandalizi ya mapendekezo ya nchi pamoja na tathmini ya mapendekezo hayo.

Katika hatua hii mambo makuu yanayofanyika ni:

- Uteuzi wa mtu mwenye sifa na uzoefu wa kutosha kuwa kama kiungo katika zoezi zima la maandalizi ya mpango wa nchi (Senior Point of Contact – POC);
- Kuanzisha utaratibu wa mashauriano na majadiliano katika maandalizi ya mapendekezo ya nchi na mpango wenyewe;

- Kuainisha vikwazo vya msingi vinavyoathiri ukuaji wa uchumi na jitihada za kupunguza umaskini na kuweka malengo na kupendekeza maeneo muhimu ya kipaumbele yatakayofikiriwa kwa ajili ya kupata msaada kutoka katika mfuko wa MCA;
- Kuanzisha kamati maalum ya usimamizi wa mpango wa nchi (A full-time core Team)
- Kuendesha majadiliano ya mara kwa mara na MCC wakati wote wa maandalizi ya mapendekezo ya nchi;
- Kuwasilisha rasmi mapendekezo ya nchi kwa MCC;
- Kama mapendekezo ya nchi yakikubalika MCC wanaanzisha kamati yao ya kushughulikia mapendekezo ya nchi husika (MCC Transaction Team – TT);
- Kamati hii inawasiliana na kuendesha mjadala na kamati maalum ya nchi husika kuhusu fursa zilizopo za ukuaji wa uchumi, kuongeza kasi katika mapambano dhidi ya umaskini na mchakato mzima wa nchi wa majadiliano na mashauriano;
- Baada ya mjadala huu, kama kamati ya MCC ikiridhika na mapendekezo ya nchi husika, inaandaa dokezo (opportunity memo) kwa kamati ya MCC ya uwekezaji (MCC Investment Committee – IC) ikiomba mapendekezo ya nchi hiyo yachunguzwe kwa kina (due diligence) kwa ajili ya kupata msaada.

2.3 Hatua ya tatu ni uchambuzi wa kina wa mapendekezo ya nchi.

Katika hatua hii, kazi kubwa inayofanyika ni kufanya uchambuzi wa kina wa shughuli/kazi zote zilizopendekezwa katika programu ya nchi. Kwa hiyo uchambuzi unahusu:-

- Mchakato mzima wa mashauriano na majadiliano ikiwa ni pamoja na uratibu wa wafadhili;
- Menejimenti ya mpango na uwajibikaji;
- Tahadhari iliyowekwa kuhusu mazingira na kinga kwa jamii (Environmental and social safeguards);
- Utaratibu wa Utekelezaji wa miradi iliyopendekezwa na mipango endelevu ya miradi hiyo. (Implementation feasibility and sustainability)

- Manufaa ya mpango mzima kwa wananchi, hasa katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Mchango wa kila mradi uliopendekezwa pia unachunguzwa; na
- Mipango ya ufuatiliaji na tathmini

2.4 Hatua ya nne ni ya majadiliano ya mwisho na maafikiano.
Katika hatua hii mambo makubwa yanayofanyika ni:

- Kamati ya MCC (TT) inaandaa dokezo na kuwasilisha rasmi mpango wa nchi na utaratibu wake wa utekelezaji kwa kamati ya MCC ya uwekezaji
- Bado kamati maalum ya nchi (Core Team) inaendelea kufanya kazi na MCC ya kufanya marekebisho ya mwisho ya mpango wa nchi kutokana na hoja zitakazojitokeza
- Kama maafikiano yakifikiwa, kamati ya uwekezaji inaomba Bodi ya MCC ipitishe mpango wa nchi husika kwa ajili ya kupata fedha kutoka katika mfuko wa MCA.

2.5 Hatua ya tano ni kupitishwa na Bodi, kusaini mkataba na kukamilisha nyaraka muhimu za utekelezaji.
Katika hatua hii shughuli kubwa zinazofanyika ni:

- MCC wanatoa taarifa kwa serikali ya Marekani (Congress) ya kusudio la kuingia mkataba na nchi husika (compact) ;
- Kama wakiafiki, Bodi ya MCC inapitisha mpango wa nchi ;
- Nchi husika na MCC wanasaini mkataba;
- MCC na kamati maalum ya nchi wanakamilisha nyaraka muhimu za kuufanya mkataba uanze kutumika kikazi ;
- Fedha za awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango wa nchi zinatolewa na utekelezaji unaanza. Mkataba unadumu kwa muda usiozidi miaka 5;
- Mpango wa ufuatiliaji na tathmini unaanza kama sehemu ya kuendeleza mashauriano na majadiliano wakati wote wa utekelezaji wa mpango wa nchi husika.

3.0 PROGRAMU YA MCA TANZANIA

Lengo kuu la programu ya Tanzania ya MCA ni kuchochea ukuaji wa uchumi, kuinua kipato na kuleta maisha bora kwa wananchi katika

ujumla wao kwa kuimarisha miundombinu ya barabara na usafirishaji, nishati na maji. Ni kutokana na lengo hili kuu, miradi iliyopendekezwa imeelekezwa kwenye:

i) Upanuzi na uimarishaji wa miundombinu ya usafirishaji ili kuchochea maendeleo ya kilimo, ujasiriamali na utalii, Tanzania Bara na Visiwani;

ii) Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa maji yenye uhakika kwa baadhi ya maeneo nchini kwa ajili ya matumizi ya majumbani na shughuli nyingine za kiuchumi mijini na vijijini Tanzania, Tanzania Bara na Visiwani;

iii) Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji na usambazaji wa nishati mijini na vijijini, Tanzania Bara na Visiwani.

Ili kupata orodha ya miradi ya kupendekezwa ilibidi kuwe na vigezo kadhaa vya kusaidia kufanya uchambuzi na hatimae kuanisha miradi yenyewe. Vigezo hivyo ni pamoja na:

(i) Miradi inayopendekezwa ni muhimu iwe na upembuzi yakinifu au angalau ule wa awali. Maandiko hayo yasiwe ya miaka mingi iliyopita;

(ii) Miradi inayopendekezwa ni lazima iwe na uwiano wa karibu sana na ukuaji wa uchumi na uondoaji wa umasikini na pia iwe na viashiria vinavyopimika;

(iii) Miradi inayopendekezwa iwe na uwiano na sekta nyingine zinazojibu hoja za ukuaji wa uchumi na uondoaji wa umasikini;

(iv) Miradi inayopendekezwa iwe ni sehemu ya miradi ya kipaumbele iliyoainishwa katika mipango na programu za sekta husika;

(v) Miradi inayopendekezwa iwe na uwezo wa kuleta manufaa kwa idadi kubwa ya walengwa kufuatana na kiasi cha fedha kitakachotumika;

(vi) Kila mradi unaopendekezwa ni lazima uwe unatekelezeka na kukamilika katika kipindi kisichozidi miaka mitano;

(vii) Kila mradi unaopendekezwa uwe umejengewa mazingira ya kuwa endelevu (sustainable). Usiwe ni mradi tegemezi bali wenye uwezo wa kujiendesha kigharama. Uwe na uhalali kiuchumi; na
(viii) Mradi unaopendekezwa usiwe chimbuko la mgongano kati ya wafadhili.

Kutokana na vigezo hivyo miradi ya usafirishaji, usambazaji maji na nishati iliyopendekezwa ni kama ifuatavyo:

Usafirishaji:

i) Barabara kutokaTunduma hadi Sumbawanga (Km 224.5)
ii) Barabara ya Tanga - Horohoro (Km 68)
iii) Barabara ya Tunduru – Songea - Mbamba Bay (Km 407.5)
iv) Barabara mbalimbali Zanzibar (Km 142.7)
v) Kiwanja cha Ndege Kigoma
vi) Kiwanja cha Ndege Mafia

Maji

(i) Bwawa la Kidunda kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji kwa Jiji la Dar-es-Salaam
(ii) Mradi wa Maji - Bukoba Mjini
(iii) Mradi wa Mambogo – Morogoro
(iv) Mradi wa Maji – Misungwi
(v) Mradi wa Maji – Bunda
(vi) Mradi wa Maji – Bariadi
(vii) Mradi wa Maji – Tarime
(viii) Mradi wa Maji – Geita
(ix) Miradi mbalimbali ya Maji Zanzibar (Unguja na Pemba)
(x) Usimamizi wa shughuli za Maji

Nishati

(i) Uimarishaji wa mtandao wa usambazaji umeme katika mikoa ya Tanga, Mbeya, Mwanza, Iringa, Morogoro na Dodoma
(ii) Malagarasi Mini - Hydro (Kigoma)
(iii) Dar es Salaam – Zanzibar Sub Marine Cable

Aina na idadi kamili ya miradi itakayofanikiwa kuingia katika programu ya Tanzania inategemea sana zoezi la uchambuzi wa kina linaloendelea hivi sasa. Kuna mambo mengi yanyochambuliwa katika zoezi hili kama ilivyooneshwa katika sehemu 2.3 hapo juu.

Kuhusu kiasi cha fedha kinachotarajiwa, maelekezo ya MCC-Washington yaliyopo ni kuwa gharama ya programu nzima iwe chini ya dola za kimarekani milioni 800 kwa kipindi chote cha miaka mitano ya mpango huu.

4.0 KAZI ILIYOFANYIKA

Zoezi la kuandaa mapendekezo ya nchi lilianza mwezi Februari 2006 kwa kuanzia na uteuzi wa Mratibu wa MCA Tanzania na maafisa wengine. Tayari mambo yafuatayo yamefanyika au yanaendelea kufanyika:

i) Ofisi ya MCA Tanzania imeanzishwa, ipo katika jengo la NSSF Water Front, ghorofa ya pili.
ii) Kamati ya Wataalam iliundwa mapema mwaka 2006 na kuanza kutayarisha mapendezo/programu ya nchi kulingana na miongozo ya MCC-Washington. Kamati hii inatoa ushauri wa kiufundi kwa Kamati Elekezi ambayo wajumbe wake ni Makatibu Wakuu wa sekta zinahusika moja kwa moja na programu hii. Wajumbe wengine wa Kamati Elekezi wanatoka katika mashirika ya hiari na sekta binafsi. Mwenyekiti wa Kamati Elekezi ni Katibu Mkuu Hazina. Kamati hii imekuwa ndiyo muhimili mkuu katika maandalizi mapendekezo /programu ya Tanzania.
iii) Rasimu ya mwisho ya programu ya nchi iliwasilishwa na Serikali ya Tanzania kwa MCC mwezi Agosti 2006.
iv) Yamekuwepo mawasiliano ya karibu sana kati ya ofisi ya Mratibu na Wataalam wa MCC-Washington.
v) Zoezi la uchambuzi wa kina wa miradi iliyopendekezwa linaendelea baada ya kupata ridhaa ya "Investment Committee" ya MCC Washington.
vi) Ni maoni ya Timu ya Wataalam wa MCC inayoshughulikia Tanzania (Tanzania Transaction Team) kuwa zoezi la uchambuzi wa kina wa programu yetu litaweza kukamilika

kufikia mwezi Juni/Julai 2007 na hivyo kuweza kusaini mkataba wa msaada kwa Tanzania mwezi Agosti/Septemba, 2007.

HATUA ZINAZOFUATA

Hatua zinazofuata ni:

- Kukamilisha zoezi la uchambuzi wa kina litakaloainisha maeneo yenye utata ambayo yatayohitaji majadiano zaidi;
- Kuendesha majadiliano katika maeneo yote yenye utata ili hatimaye kufikia maafikiano kuhusu utaratibu mzima wa uendeshaji wa programu, miradi na vipengele muhimu vitakavyoingia katika mkataba wa makubaliano na utaratibu wa ufuatiliaji na kutoa ripoti muhimu za utekelezaji;
- Kusaini mkataba na kukamilisha nyaraka zote muhimu zinazohusu taratibu za utekelezaji;
- Kuanza rasmi kupokea fedha za uendeshaji wa miradi na kusimamia utekezaji wa miradi itakayofadhiliwa chini ya mfuko huu.